



## Hatokuwa na imani mmoja wenu mpaka yawe matamaniao yake ni yenye kufuata yale niliyokujua nayo

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Muhammadi Abdallahi bin Omari -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani ziwe juu yake-: "Hatokuwa na imani mmoja wenu mpaka yawe matamaniao yake ni yenye kufuata yale niliyokujua nayo".

[Amesema Nawawi: Hadithi hii ni sahihi] [Imepokelewa na katika kitabu cha Al-Hujjah kwa msururu sahihi wa wasimulizi]

Amebainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa mwanadam hawezi kuwa muumini mwenye imani kamili ya wajibu mpaka mapenzi yake yafuate yale aliyokuja nayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake miongoni mwa amri na makatazo na mengineyo, ayapende aliyoamrisha, na ayachukie aliyokatazwa.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66535>

